
# MAONGOZI YA NYAYO KAMBE-RIBE

na S.A. AL-ISMAILLY

VIONGOZI NA wazee wa Kambe Ribe wamepitisha kauli moja kumuunga mkono Bwana Gabriel Kiinda Ngala katika Uchaguzi ujao wa Bunge ili kuleta maongozi thabiti ya Nyayo huko Kilifi kusini kwa jumla na kumaliza mtindo wa kutokuwa na maendeleo kutokana na viongozi wachoyo na walafi.



• MZEE Karani Rua

Pendekezo hilo limetolewa na Mwenyekiti wa Kanu sehemu hiyo Bwana Karani Rua (pichani) ambaye pia ni Mwenyekiti wa shule ya Msingi ya Pangani.

Katika matamshi yake Bwana Karani Rua alisema "viongozi wa sehemu hiyo Mabwana Patrick Mambo; Samuel Chivatsi, Pekeshe Ndeje Ndara, Shadrak Mazera, Samson Mgogoro, Ali Muturi Mazera na Mabwana Mohamed Kubahatisha, Kesi Katama na Shadrak Kandoro wamekata shauri zamani kufuata maongozi ya Nyayo ya Mtukufu Rais Moi ili kuleta maendeleo ya haraka sehemu yao".

Mzee Karani Rua alifahamisha "watu wa Kambe Ribe wanafahamikiwa vizuri na vile hali ilivyo Kenya na kwamba hawatababaika tena kwani kutofuata maongozi ya Nyayo ni kurudi nyuma na kupingana na wakati".

Alisema "Watu wanafahamu jinsi makundi ya wapinzani walivyojaribu kubadilisha katiba ya Taifa hili, walipojaribu kupinga kuchaguliwa kwa mtukufu Rais Moi kuwa Rais wa Taifa na chama chetu kinachotawala, na vile vile makundi ambayo yalijitokeza kumpinga makamu wa Rais Kibaki asiwe Makamu wa Rais wa Chama cha Kanu na serikali".

Alisema "Mengi ya upinzani hayakufua dafu, na kwamba leo Kenya imebahatika kuwa na Viongozi wapenda Umoja, furaha, amani na maendeleo ya Kenya yote".

Bwana Karani Rua alikuwa akiongea katika Mkutano wa kupokea zawadi za vitabu vilivyotolewa na Umoja wa Roteract Club ya Mombasa mwishoni mwa wiki iliyopita huko Pangani Kambe Ribe.

Alimpongeza Bwana Gabriel Ngala kwa kufanya bidii kuwaombea misaada watu wake watoke ujingani kwani "kuomba si kuiba", alisema.

Mwenyekiti wa Roteract Club Mombasa Bwana Chaky Vaghela alisema Umoja wao utaendelea kuunga mkono mipango ya elimu mashambani. Aliandamana na baadhi ya wanachama wa umoja wake pamoja na Bwana Saleem Mamujee na Bwana Vijay Shikotra.

Akihutubia sherehe hiyo Bwana Gabriel Ngala alisema "Maongozi ya Nyayo yana lengo la kuleta maendeleo kote nchini na kwamba watu wasirudi nyuma ya wakati kwani majuto kila siku ni mjukuu".

Alisema "Kilifi kusini imekuwa nyuma kwa mengi lakini sasa ni lazima kuzifuata Nyayo za Rais Moi pale zilipo".

Wazee wa sehemu hiyo wakiongozwa na Mzee Karani Rua walipeleka maombi Mtukufu Rais au Makama wake awatembelee watu wa Kilifi Kusini.

Mwalimu Mkuu wa shule ya Pangani Mwalimu Gilbert Murira aliupongeza moyo wa usaidizi uliongozwa na Bwana Gabriel Ngala wa kuletea watoto misaada kutokana na marafiki.

Alisema msaada huo wa vitabu vya Maktaba ni wa kwanza kabisa katika historia ya sehemu hiyo. Alisema kila mara ilikuwa ni serikali tu inayotoa misaada.



*KAMPUNI YA Wamisri nchini Kenya El Naser hivi juzi ilipakia shehena za majani ya chai katika meli ya 'Hellenic Torch' bandarani Kilindini kuelekea Misri. Baadhi ya shehena nyingine ilikuwa kahawa ya Kenya, ngozi na bidhaa nyingine.*

*Akishuhudia upakizi wa bidhaa hizo Melini, Meneja wa Kampuni hiyo yenye matawi yake Mombasa na Nairobi Bwana Muhsin Halil (anayeonekana pichani) alisema ipo nafasi kubwa zaidi kati ya Kenya na Misri katika shughuli biashara. Alisema Kampuni yao inaendelea kudumisha moyo wa ushirikiano kati ya Misri na mataifa ya Afrika Mashariki. Meli hiyo hapo awali ilikuwa imeshabeba shehena za bidhaa nyingine kutokana na bandari ya Tanzania huko Dar es Salaam.*

## SAHAU YANISUMBUA

*Nakugotea swahibu*
*Nichapia yasighibu*
*Nitabiriwa maswibu*
*Illi mnipe yakini*

*Nawauliza wajuzi*
*Mubaini ndwe hizi*
*Nisipatwe jinamizi*
*Nijue nidawa gani*

*Mfano kitu meeka*
*Pindi nikihitajika*
*Akili huvurujika*
*Malenga niambieni*

*Huranga nakutafuta*
*Niwapi nitakikuta*
*Hushika tama kajuta*
*Nitumie njia gani*

*Tabia ya kuzubaa*
*Asili sikupumbaa*
*Sijui ni gani baa*
*Mujuwao nijibuni*

*Naupata hadi kwacha*
*Navila sivyakuchacha*
*Siumwi hata ukucha*
*Kumekucha nijubuni*

*Moyo wangu ubaridi*
*Wala sina itikadi*
*Wa furaha nimaujudi*
*Msinipuze jamani*

*Mawazo yakufikiri*
*Hilo nnalikariri*
*Akili yangu bukheri*
*Niambieni jamani*

*Natosheka nipatacho*
*Kikwangu nikipendacho*
*Wenzangu mengiwa kicho*
*Wabara hadi wapwani*

*Tamati natia nanga*
*Sahau yanibananga*
*Jitokezeni malenga*
*Nijibuni wahisani*

*Muhariri muhisani*
*Ijapo kua pembeni*
*Yalonitika jamani*
*Iniondoke sahau.*

*Wazuo namburugani*
*Nitume dawa gani?*
*Munitoe sahauni*
*Iyondowao sahau*

*Mahala penye amani*
*Nisingie tafutoni*
*Mara hua sahauni*
*Dawa ya hii sahau*

*Sizumbui asilani*
*Sielewi abadani*
*Nikashukuru manani*
*Iniondoke sahau?*

*Mimi sina aswilani*
*Kutwa nimo shughulini*
*Sahau yanimakini*
*Dawa ya hii sahau*

*Usingizi wa makini*
*Vilivyo na vitamini*
*Sina dosali mwilini*
*Ipate kwenda sahau*

*Sina kinyongo jamani*
*Moyo wangu umakini*
*Kwangu haikosekani*
*Itabirini sahau*

*Yakupita ukomoni*
*Halipiti kikomoni*
*Itimamu ubongoni*
*Iniondoke sahau*

*Cha mwengine sitamani*
*Roho sina walakini*
*Sahau yanishaini*
*Nambieni yasahau.*

*Nilipo nikituoni*
*Isha huona jioni*
*Sahau imtoke nuni*
*Iniondoke sahau.*

na BI-N. OMAR, MCHA MUNGU, MOMBASA

# Pilikapilika za uchaguzi

na S.A. AL-ISMAILLY

WAKATI PILIKAPILIKA za matayarisho ya uchaguzi mkuu zinapoendelea nchini Kenya, Mbunge wa Kilifi Kaskazini mpendwa Bwana Noah Katana Ngala ambaye amedhihirisha maongozi halisi ya Nyayo yuwaonekana kuongoza bila upinzani kwani mpaka sasa ni mtu mmoja tu ambaye anatarajiwa kumpinga katika Uchaguzi mkuu wa Bunge ujao.

Kiti cha Kilifi Kusini kinapiganiwa na watu wapatao watano wakati Bwana Gabriel Kiinda Ngala akiwa yuko mbele kabisa kwa maongozi ya Nyayo ambayo wananchi wa Kilifi Kusini wameamua kuyafuata kufa kupona.

Katika sherehe moja Wananchi wa sehemu hiyo wametoa mwito kwa Mtukufu Rais Moi kutembelea sehemu hiyo baada ya uchaguzi mkuu ili wananchi wa Kilifi Kusini waweze kumuona binafsi na kuchangia mipango ya maendeleo katika sehemu hiyo ili kufufua maendeleo Kilifi Kusini.

**MADIWANI:**

Jumla ya watu 116 wamejitokeza kupigania viti vya Udiwani Mombasa. Mchuano mkali unasemekana utatokea Ward ya Majengo kati ya aliyekuwa Mayor wa Mombasa Bwana Rajab Sumba na mwenyekiti wa Chama cha Wenye Matatu Bwana Soud Coca.

Kiti cha Mji wa kale Bi Shue Soud, Bwana Hassan Shariff Abdalla Abubakar (Kimwinyi) na Bwana Babilo watachuana katika kiti hicho.

Wengine ni pamoja na Maalim Hussein ambaye ni shujaa wa siasa sehemu za Tononoka, Bwana Seif Kajembe huko Mikindani, Omar Chuka ward ya Changamwe, Bin Shahbal ward ya Floringi, na kadhalika.

Bwana Daniel John Ngala anaongoza katika wardi ya Chonyi, huko Kilifi Kusini, Bwana Mohammed Fadhil katika ward ya Jibana.

Bila ya shaka wananchi wa Mombasa watafanya makini za kutosha kuona kwamba madiwani wanaofaa watachaguliwa iil kuepukana na hatua za kuvunjiliwa mbali kwa baraza kutokana na mizozano. Mombasa sasa inakaribisha hatua za kuufanya mji huo kuwa Mji Mkuu.



• BWANA Ezra Imbahale

# SHARIFF APEWA PONGEZI

na S. A. AL-ISMAILLY

KWA niaba ya Umoja wa Maragoli Development Association Mombasa Bwana Ezra Imbahale wa Mombasa ametoa shukurani zake kwa Mheshimiwa Mbunge wa Mombasa Central Mhe. Shariff Nassir ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kanu Mombasa kwa usaidizi wake wa hivi majuzi katika mkutano wa Kuchangia mipango ya maendeleo huko Vihiga.

Kwa niaba ya Umoja wake Bwana Ezra Imbahale vile vile amemshukuru Mbunge wa Vihiga ambaye pia ni Katibu wa Kanu huko Kakamega Mheshimiwa Bwana Mussa Mudavadi kwa kuwasili Mombasa ili kushiriki katika Mkutano ambao ulichangia zaidi ya shule 20 za msingi na za Harambee huko Vihiga.

Alisema Mheshimiwa Bwana Mudavadi amepata imani ya watu wake wote wa Vihiga.

## KWA UFUPI

**KILIFI:**

**Walimu waliyohitimu mafunzo ya SI au Graduates wanatakikana katika shule ya Harambee ya Jaribuni Wilayani Kilifi Kaskazani. Jumla ya nafasi mbili zipo wazi.**

**Walimu hao watalipwa kulingana na taratibu za serikali na Teachers Service Commission. Maombi yapelekwe kwa Mwenyekiti wa Jaribuni Harambee Secondary School, c/o Sheikh Salim Said Maamiry, Sanduku la Posta 12, Jaribuni Kilifi District.**

**MOMBASA:**

**Kiliniki ya bure ya kuzuia uzazi katika wanyama ilafunguliwa katika ukumbi wa Tononoka na chama cha K.S.P.C.A. kuanzia tarehe 28/9/79 mpaka tarehe 30/9/79.**

**Kutokana na msimamizi mkuu wa S.P.C.A. Mombasa Bwana Francis Kiania wenye paka na mbwa kwa mfano wanaweza kuwapeleka huko na ni lazima wawe wameshadungwa sindano za kuzuia ugonjwa wa kichaa. Sindano hizo ikiwa bado italazimu kutolewa kwa shillingi 2/= tu. Maelezo zaidi piga simu nambari 23370 Mombasa.**

**MOMBASA:**

**Wafanyi biashara mjini Mombasa wakiwa pamoja na wauzija wa mawe yenye thamani na wenye cinema ambao leseni zao zitamalizika kati ya tarehe 31/12/79 na mwezi wa March 31 mwaka ujao wameshauriwa kukata leseni zao mara moja.**

**Afisa mkuu wa biashara Pwani Bwana Ogana alisema "Ni sawa hasa kwa wakati huu wafanyi biashara kupeleka maombi ya leseni zao za mwaka ujao wa 1980".**

**KWALE:**

**Wakaazi wa Gadini huko kwale wamekata shauri ardhi zao zipimwe na kuambatana na mipango ya maendeleo ya serikali. Wakaazi wa sehemu hiyo hapo awali walidai kwamba baadhi ya watu kutoka sehemu nyingine waliingilia mpango huo kutaka kuuharibu.**

**MOMBASA:**

**Baraza la mji wa Mombasa limetoa jumla ya shillingi 25,000 kwa makao kadha wa kadha ya wasiojiweza mjini Mombasa katika mpango wa Idd el Fitr na Christmasi.**

**MOMBASA:**

**Makao mapya ya Islamic Centre yatarijiwa kufunguliwa hapo kesho jumaamosi tarehe 22/9/79. Makao hayo ni mali ya umoja wa akina mama ya Mombasa Women Institute Kiongozi wa umoja huo ni Bi Shemsa Muhashamy Maarufu mwanakutani.**


## Coastweek ** JEMBE

*SWAHILI CROSSWORD NO. 45*

*KWENDA KULIA:*
1. Si moto lakini moshi hutoa
5. Sehemu ya angani
6. Kusanya na weka pamoja
7. Kufanya jambo jema kwa kujionesha
8. Natoa ahadi
11. Ama
12. Kimoja katika vifaa vya seremala
15. Kinyume cha neno 'nje' kwa Kimombo
17. Toa harufu mbaya
18. United Nations
19. Jina la kike
20. Tamko la kukataa

*KWENDA CHINI:*
1. Nchi huru Afrika
2. Via, kupevuka kwa kukosa nguvu kwa maradhi
3. Kupata faida
4. Jina la Kijaluo
5. Fanya bidii
9. Hati ya pesa
10. Toboa kwa kitu chenye ncha
13. Azidi kimo
14. Fanyiana arusi
16. Hupatikana katika mzinga wa nyuuki

JEMBE
UNGA SAFI NO. 1
WA MAHINDI




JINA.................................

SANDUKU LA POSTA.......................

.........................................

**Washindi wa Fumbo la Kujaza Maneno No. 43:**

[1] Salwa Ali Said, Sanduku la Posta 82868, Mombasa,

[2] A. S. Mohamed, Sanduku la Posta 84506, Mombasa,

[3] Mohammed Ali Salim, Sanduku la Posta 92551, Msa.

Washindi waombwa wafike afisini mwa *COASTWEEK*

**MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO. 43**

**KWENDA KULIA:**

2. PEA, 5. DK, 7. AWALI, 8. UOI, 10. PINGANA, 11. MKOMA, 13. AYA, 15. UNA, 17. ANDAO, 20. KIPANGA, 21. AOI, 22. GOMBI, 23. AA, 24. AAA

**KWENDA CHINI:**

1. NAAM, 2. PAPO, 3. ELIMU, 4. AINA, 5. DUAA, 6. KONYOA, 9. EAA, 12. KANIOA, 14. ONGOA, 15. UKA, 16. APEA, 17. ANGA, 18. DAMA, 19. OLEA.

### Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa.

Washindi watatu wa kwanza kila mmoja atapatiwa 'T'-shirt moja ya Jembe.

Shindano hili limedhaminiwa na *COASTWEEK LTD* pamoja na ATTA LTD, Mombasa.

Jawabu za fumbo hili lipelekwe kwa muhariri, *COASTWEEK*, Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya, siku ya Alhamisi tarehe 27.9.79 saa sita mchana shindano hili litakuwa mwisho.